

# *Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo*

## **1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01-10 JUNI, 2026 NA MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11-20 JUNI, 2026.**

### **1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA TAREHE 01-10 JUNI, 2026.**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilisababisha ukanda mvua kuendelea kusogea kuelekea kaskazini zaidi na kuwepo katika maeneo ya kanda wa Ziwa Victoria. Vilevile, upepo wa bahari wenye unyevunyevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani ulikuimarisha kwa vipindi, mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani hususan yale yaliyopo nyanda za juu kaskazini mashariki.

### **1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 JULI, 2026.**

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache ya ukanda wa Ziwa Victoria na vipindi vya mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki. Pia vipindi vya mvua kubwa viliripotiwa katika ukanda wa pwani ya kaskazini.

## **2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11-20 JUNI, 2026.**

### **2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 JUNI, 2026.**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhohofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua kuendelea kusogea kuelekea kaskazini zaidi nje ya nchi yetu. Vilevile, upepo wa bahari wenye unyevunyevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani unatarajiwa kuimarisha kwa vipindi mifumo isababishayo

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)

mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani hususan yale yaliyopo nyanda za juu kaskazini mashariki.

## **2.2 MWELEKEO WA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11-20 JUNI, 2026.**

**Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Mvua zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Hali ya ukavu inatarajiwa.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Imetolewa na:

## **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

---

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)